


Bibilia ya watoto
Inawalettea

Jeshi
Dogo la
Gideoni




Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Janie Forest;
Alastair Paterson
Imerekebishwa na: Ruth Klassen
Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2022 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.






Baada ya YOSHUA
kufa, watu wote wa
Israeli hawakumtii
Mungu na wakamuacha
katika maisha yao.
Mungu akaruhusu
majirani zao
Wamidiani
kuyateketeza

mazao na nyumba
za Israeli. Ilibidi
Waisraeli waishi
kwenye mapango.




Muisraeli mmoja, Gideoni, lazima alikuwa na sehemu ya siri kwa ajili ya kupanda ngano. Alipepeta ngano ndani ya shinikizo lililojificha chini ya mti mkubwa.


Wamidiani hawakujua mahali hapo - lakini Mungu alipajua! Mungu alituma Malaika akiwa na ujumbe kwa ajili ya Gideoni.




Mungu alimtaka Gideoni aharibu sanamu ya mungu wa uongo ya baba yake na kumjengea Mungu wa kweli madhabahu. Ingawa Gideoni aliogopa kwamba watu wa mji wake watamuua, alifanya kile Mungu alichomuagiza.



Mungu pia alitaka Gideoni aongoze jeshi la Israeli kupigana na Wamidiani waovu. Lakini Gideoni aliogopa. Akaomba ishara maalumu kuthibitisha kama Mungu alikuwa pamoja naye. Kisha akalaza ngozi ya kondoo juu ya ardhi.







Gideoni
akaomba,
"Kama
ukiwapo
umande juu ya
ngozi tu, na nchi yote ikiwa
kavu, basi, hapo ndipo nitakapojua
ya kuwa utawaokoa Israeli kwa mkono wangu,
kama ulivyosema." Asubuhi, nchi ilikuwa kavu,
lakini **NGOZI ILIKUWA IMELOWA MAJI!**




Bado Gideoni akawa na wasiwasi. Sasa akataka Mungu atume umande kwenye nchi lakini sio kwenye ngozi. Asubuhi iliyofuata - nchi ikawa na unyevu, lakini **NGOZI IKAWA KAVU!**



Gideoni alianza na jeshi la watu 32,000.
Mungu akalipunguza hadi watu 300 tu.
Mungu hakutaka Israeli waseme "Mkono
wangu mwenyewe ndio ulioniokoa." Mungu
pekee ndiye alikuwa Mwokozi wa Israeli.



Kwa vile Mungu alijua bado Gideoni anaogopa, akamfanya asikie kwa siri askari mmoja Mmidiani akimwambia mwingine kuhusu ndoto ya ajabu. Katika ndoto, mkate wa shayiri uliangukia hema ya Wamidiani na kuiharibu.




Huyo mlinzi mwingine akaogopa sana.
Akasema, "Huu ... ni upanga wa Gideoni ..."
Gideoni aliposikia ndoto na maana yake,
akajua Mungu anakwenda kumpa ushindi.




Gideoni akapanga mashambulizi ya usiku. Alimpa kila askari tarumbeta, na mitungi isiyo na maji na mienge ndani ya hiyo mitungi.


Wakazingira jeshi la Wamidiani.



Gideoni alipowaonyesha ishara, maaskari wakapiga tarumbeta, wakaivunja mitungi na kuwasha mienge yao. Hiyo kelele sasa! Huko kuchanganyikiwa! Wamidiani kwa woga wakainuka na kukimbia.



Baada ya huu ushindi mkuu, watu wa Israeli wakamsihi Gideoni awatawale. Gideoni akawajibu, "Sitawatawala. BWANA atatawala juu yenu." Alijua kwamba ni Mungu tu mwenye haki ya kutawala maisha ya watu.



Jeshi Dogo la Gideoni

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Waamuzi 6-8

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130





Mwisho

15



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

